
Jarida la

# SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz | Mwezi Februari 2024 | Toleo la 14 | Halmashauri ya Siha



# RC KILIMANJARO AZUNGUMZA NA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI YA SIHA



**Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu akizungumza wakati wa kikao kazi na menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha 27 Februari,2024 katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri.**

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu ameipongeza Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ambayo inayochangia kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mhe. Nurdin Babu ametoa pongezi hizo Februari 27, 2024 wakati wa kikao kazi na Menejimenti hiyo kilichofanyika katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ambapo amesema nguvu zaidi inatakiwa ili kufikia bajeti ya mapato ya ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024

Amesema robo ya kwanza na ya pili ya mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Siha imeshika nafasi ya pili katika Mkoa wa Kilimanjaro kutokana na juhudi za pamoja za Mkurugenzi Mtendaji, wakuu wa Divisheni na Vitengo pamoja na Watumishi wote.



*Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe Nurdin Babu (katikati) akiwa kwenye kikao kazi na Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji Dkt Haji Mnasi ( kulia) Februari 27, 2024.*





*Wajumbe wa kikao kazi cha Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu Februari 27, 2024.*



*Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu akikagua miundombinu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa Kilimanjaro (Kilimanjaro girls) Februari 27, 2024 alipotembelea shule hiyo.*



**Baadhi ya miundombinu ya Madarasa, Maabara, Mabweni na Nyumba za Walimu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa  Kilimanjaro (Kilimanjaro Girls secondary school) iliyopo Kata ya Gararagua Wilaya ya Siha.**

## MSITUMIE MADARAKA VIBAYA – DKT. TIMBUKA DC SIHA



*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe Dkt Christopher Timbuka akizungumza Februari 08, 2024 katika kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha*

Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka amewaelekeza Watendaji wa Kata na Vijiji kufanya kazi kwa weredi na haki huku wakifuata sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Mhe. Dkt Timbuka ametoa maelekezo hayo Februari 08, 2024 wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha ambapo amewataka watendaji kuacha kutumia madaraka yao vibaya.

Amesema ikibainika mtendaji ametumia madaraka yake vibaya kwa lengo la kuwaumiza wananchi, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ili kukomesha tabia hiyo kwa kulinda na kudumisha usalama na amani.

“Tusitumie madaraka yetu vibaya, na unapoyatumia vibaya na kusababisha uvunjifu wa amani sisi tutakushughulikia wewe, lakini tusingependa tufikie huko, fanyeni kazi kwa weredi kwa kufuata utaratibu uliopo” amesema Dkt Timbuka.

Kwa upande wake, Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Siha, Mrakibu Msaidizi (SSP) Zakia Shuma amewaomba watendaji kutokuwa sababu ya wananchi kukosa haki yao ikiwemo dhamana kwani hali hiyo inalichafua Jeshi la Polisi.

“Sheria za dhamana zipo wazi kabisa na wote kama watendaji wa Serikali tunazijua, sasa inapotokea mwananchi anakosa haki yake kwa sababu mtendaji haujampa barua ya kibali inanisitikisha, niwaombe muweke uzalendo mbele wa kuwahudumia wananchi kwa kufuata sheria za nchi” amesema SSP Zakia Shuma.



*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (Kulia) akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt. Haji Mnasi (kushoto) Februari 08, 2024 wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha*





*Baadhi ya wajumbe wa kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Wilaya ya Siha kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Februari 08, 2024*

# DED SIHA APONGEZWA KWA USIMAMIZI MZURI WA MIRADI



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Siha Mhe. Duncan Urassa (kwanza kulia mbele) akiongoza kamati ya edha, Uongozi na Mipango kukagua mradi wa ujenzi wa shule ya Wasichana Mkoa Kilimanjaro wakiwa katika kijiji cha Mawasiliano Kata ya Gararagua wakati wa ziara ya kamati hiyo kukagua miradi ya maendeleo Februari 02, 2024.*

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa amempongeza Dkt. Haji Mnasi Mkurugenzi Mtendaji kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Wilaya ya Siha.

Mhe. Urassa ametoa pongezi hizo Februari 02, 2024 wakati wa ziara ya kamati ya fedha, uongozi na mipango walipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya Wilaya ambapo amesema kazi iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa Kilimanjaro (Kilimanjaro Girls) ni nzuri na thamani ya fedha inaonekana kwenye mradi.

Amesema Mkurugenzi pamoja na timu yake imefanya kazi kwa ufanisi ambapo mpaka sasa shule hiyo imepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro na wanasoma katika mazingira bora na salama.

“Kwa kazi iliyofanyika hapa Mkurugenzi unastahili kupongezwa, wakati tunaanza utekelezaji wa mradi huu watu hawakutegemea kama wanafunzi wangeripoti na kuanza masomo mara moja lakini wewe na timu yako pamoja na Mkuu wa Wilaya mkahamishia nguvu hapa, na sasa wanafunzi wameripoti na wapo darasani” amesema Mhe. Urassa.

Kwa upande mwingine Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Haji Mnasi,amemshukuru Mwenyekiti wa Halmashauri na waheshimiwa madiwani kwani ushauri na mapendekezo wanayotoa yamekuwa yakichangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.





*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa na Mkurugenzi Mtendaji  Dkt. Haji Mnasi, wakiiongoza kamati ya fedha uongozi na mipango kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana mkoa wa Kilimanjaro Februari 02, 2024.*





*Muonekano wa nyumba ya mkuu wa shule (kulia) na nyumba ya watumishi (kushoto) katika shule ya Sekondari ya wasichana Mkoa wa kilimanjaro.*





*Muonekano wa jengo la kupumzikia (sick bay) (kulia) na baadhi ya vyumba vya Maabara na madarasa (kushoto) katika shule ya sekondari ya wasichana Mkoa wa Kilimanjaro*

**KAMATI YA FEDHA YARIDHISHWA NA MAENDELEO YA UJENZI WA BWENI SIKIRARI SEKONDARI**



*Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Noel Mollel (kwanza kushoto) akizungumza baada ya kamati ya fedha, uongozi na mipango kukagua maendeleo ya ujenzi wa bweni moja katika shule ya Sekondari sikirari Kata ya Donyomurwak.*

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha imeipongeza Menejimenti na viongozi wa kata ya Donyomurwak kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa bweni moja la wananfunzi wa kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari sikirari.

Kamati ya fedha imetoa pongezi hizo Februari 05, 2024 baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa bweni unaotekelezwa kwa fedha za Serikali kuu kupitia mradi wa EP4R Shilingi Milioni 130 ambapo makamu mwenyekiti wa halmashauri amesema baada ya kutembelea kamati inapongeza kazi imefanyika vizuri na thamani ya fedha inaoenekana.

Makamu Mwenyekiti Mhe. Noel Mollel ameshauri nguvu iliyotumika wakati wote iendelee ili kuhakikisha umaliziaji wa bweni hilo unafanyika kwa ubora na ufanisi unaotakiwa.

“Kwanza tuipongeze menejimenti, mradi ni mzuri tunaona kazi ilivyofanyika kuanzia hatua za awali mpaka sasa wakati wa umaliziaji, naomba kutoa wito kuendeleza nguvu mliyoanza nayo ili umaliziaji ufanyike kwa ubora huu huu tuliouona leo” amesema Makamu Mwenyekiti Mhe. Noel Mollel.

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz




*Muonekano wa jengo jipya la  bweni   la kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari Sikirari linalotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu  shilingi milioni 130*



*Wajumbe wa kamati ya fedha uongozi na mipango wakitoa maoni baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa bweni la kidato cha tano na sita katika shule ya Sekondari Sikirari linalotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu shilingi milioni 130.*

# DED SIHA AWATAKA WATENDAJI KUENDELEA KUSIMAMIA MAPATO NA MIRADI YA MAENDELEO




*Mkuu wa wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (Kulia) akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt. Haji Mnasi, (kushoto) Februari 08, 2024 wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Wilaya ya Siha Dkt. Haji Mnasi amewaelekeza watendaji wa Kata na Vijiji kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo wanayoyasimamia.

Dkt.Mnasi, amesema hayo Februari 08, 2024 wakati wa kikao kazi cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024 zitakazozinduliwa katika Mkoa wa Kilimanjaro tarehe 02 Aprili,2024.

Amesema Serikali imeipatia Wilaya ya Siha fedha nyingi za miradi ya maendeleo hasa sekta ya elimu na afya hivyo ni vizuri watendaji wakaendelea kusimamia kwa karibu miradi hiyo.

"Niendelee kuwaomba watendaji wa Kata na Vijiji muendelee kusimamia kwa ukaribu ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mnayoyasimamia ili kwanza tufikie mapema makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani na miradi ikamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa" amesema Mkurugenzi Mtendaji Haji Mnasi, PhD










*Baadhi ya wajumbe wa kikao cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Mwaka 2024 wakiwa kwenye kikao hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Februari 08, 2024.*





*Mwakilishi wa Benki ya Uchumi Tawi la Siha akizungumza wakati wa kikao cha maandalizi ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru Mwaka 2024 wakiwa kwenye kikao kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Februari 08, 2024.*

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

## TOENI ELIMU KWA WANANCHI KUJIKINGA NA MAGONJWA YA MLIPUKO– MHE URASSA



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa akizungumza Februari 09, 2024 wakati wa kikao cha kamati ya huduma za afya ngazi ya jamii (Primary Health Care) cha maandalizi ya kampeni ya kitaifa ya chanjo ya Surua Rubella.*

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa ameiagiza idara ya afya kwa kushirikiana na Watendaji wa Kata na Vijiji, Wenyeviti na Viongozi wa dini kutoa elimu na kuongeza nguvu ya kufanya usafi katika maeneo ya biashara hasa za vyakula ili kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu.

Mhe. Urassa ametoa agizo hilo Februari 09, 2024 wakati wa kikao cha kamati ya huduma za afya ngazi ya jamii (Primary Health Care) cha maandalizi ya kampeni ya kitaifa ya chanjo ya Surua Rubella na kuelezea utekelezaji wa miradi ya lipa kulingana na matokeo (EP4R) inayotekelezwa katika ngazi ya jamii, Zahanati, idara ya maji na elimu msingi.

“Wakati mwingine inatia kinyaa unapopita eneo wanapouza chakula, ukiona maji wanayotumia kuoshea vyombo ni hatari kwa afya za watumiaji, ni vizuri maafisa afya wakapita katika maeneo hayo kukagua na kuchukua hatua kwa wanaokiuka miongozo ya afya” amesema Mhe. Duncan Urassa

“Kwa sasa tunaweza kuona hali ni nzuri lakini kipindupindu kikiibuka biashara hizi zote hazitafanyika kabisa, sasa ili tusifikie huko ni vyema nguvu ya kufanya usafi na ufuatiliaji ikaongezwa na ofisi ya mkurugenzi inatakiwa kufuatilia kwa ukaribu uboreshaji wa eneo la kutupia taka (Dampo)” ameongeza Mhe Urassa.




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi, PhD akifungua Baraza Maalumu la Wafanyakazi ili kupitia na kujadili Mpango wa Bajeti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 lililofanyika katika Ukumbi Mikutano wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Januari 22, 2024.*





*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakitoa mchango kwenye baraza maalumu la kujadili Mpango wa Bajeti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Januari 22, 2024.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakiwa kwenye Baraza maalumu la kujadili Mpango wa Bajeti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 lililofanyika katika Ukumbi Mikutano wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Januari 22, 2024.*

# SERIKALI YAPONGEZWA KWA KUBORESHA MAZIMGIRA YA UTOAJI WA ELIMU WILAYANI SIHA



*Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari Mwalimu Naomi Swai akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Februari 14, 2024 wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha Afisa elimu Sekondari na Walimu wa Taaluma katika shule za Sekondari kilichofanyika ukumbi wa kituo Cha Walimu (cluster) Sanya Juu.*

Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan imepongezwa kwa kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma za elimu Sekondari Wilaya ya Siha kwa kuongeza na kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

Pongezi hizo zimetolewa Februari 14, 2024 na Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari Mwalimu Naomi Swai kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt.Haji Mnasi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha Afisa elimu Sekondari na Walimu wa Taaluma katika shule za Sekondari, kikao kimefanyika katika kituo cha Walimu (cluster) Sanya Juu.

"Kipekee tunashukuru Uongozi wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Siha ukiongizwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Siha Mhe. Duncan Urassa pamoja na Madiwani wote kwa Uongozi mzuri ulioleta mafanikio mengi ya elimu Wilayani Siha" amesema mwalimu Naomi Swai.

"Sambamba na hilo walimu wetu wanaendelea kupewa mafunzo endelevu kazini kwa masomo ya sayansi hali inayowafanya wanafunzi kupenda masomo ya sayansi" ameongeza Mwalimu Naomi Swai.

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz




*Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari Mwalimu Naomi Swai (katikati) akiwa pamoja na maafisa elimu sekondari Herman msasa (kulia) na Joyce Lukiko (kushoto) kwenye kikao kazi cha Afisa elimu Sekondari na Walimu wa Taaluma katika shule za Sekondari Februari 14, 2024 katika ukumbi wa kituo Cha Walimu (cluster) Sanya Juu.*





*Baadhi ya walimu wa taaluma katika shule za Sekondari Wilaya ya Siha wakiwa kwenye kikao kazi kilichofanyika Februari 14, 2024 katika ukumbi wa kituo Cha Walimu (cluster) Sanya Juu, ili kuweka mikakati bora na fanisi ya kuimarisha ufaulu wa wanafunzi katika Wilaya ya Siha.*




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akifuatilia Mkutano wa Baraza la waheshimiwa Madiwani katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri februari 20, 2024.*






*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe Duncan Urassa akizungumza kwenye Baraza la Waheshimiwa Madiwani kipindi cha robo ya pili mwaka wa fedha 2023/2024 lililofanyika februari 20, 2024*





*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt Haji M. Mnasi akizungumza kwenye Mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani februari 20, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri.*





*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mhe. Duncan Urassa (katikati) akiongoza mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani akiwa na makamu mwenyekiti mhe Noel Mollel (kushoto na Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Haji Mnasi (kulia) uliofanyika februari 20, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri.*



*Waheshiwa madiwani wakiwa kwenye baraza lililofanyika februari 20, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri.*

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

**FURSA ZA UTALII KATIKA WILAYA YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO**



*Maporomoko ya West Kilimanjaro, Fahari ya Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro*



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha**
**5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha**
**Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677**
**Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

**Tunapatikana**